# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/2 KIDATO CHA KWANZA

# MUHULA WA KWANZA 2024

**1. INSHA ALAMA 20**

Hii ni insha ya hotuba

Vipengele muhimu vya insha ya aina hii viweze kuzingatiwa

Vipengele hivi ni:

1. **Muundo**

i) Kichwa
Kichwa kibainishe kuwa ni hotuba
Kibainishe hatibu kwa kutaja jina au cheo.
Kionyeshe hadhira itakayohutubiwa pamoja na lengo la hotuba
Kionyeshe tarehe itakapotelewa

ii) Utangulizi
Huhusisha maamkizi kwa hadhira
Hutambua kwa kutaja waliohudhuria
Huanza kutaja walio na vyeo vya juu hadi wale wa vyeo vya chini
Hutoa shukrani kwa fursa aliyopewa
Hutaja mada

iii) Mwili wa hotuba
Hii ndiyo sehemu ya maudhui ya insha.
Hujumuisha aya mbalimbali kulingana na hoja mtahiniwa anazungumzia.

iv) Hitimisho
Huu ni muhtasari wa maelezo yatakayosemwa mwishoni

2. **Maudhui**

Hoja zifuatazo ziweze kujitokeza:

i) Kupiga kelele darasani
ii) Kutozingatia usafi wa mwili
iii) Kukosa kuvalia sare ya shule
iv) Kuchelewa kuingia darasani
v) Kutokamilisha kazi ya ziada
vi) Kutoroka shule
vii) Matumizi ya simu shuleni
viii) Kuiba mitihani kushiriki matumizi ya dawa za kulevya
ix) Kuwa na mahusiano ya kimapenzi shuleni
x) Kutohudhuria vipidi vyote darasana
xi) Kupigana shuleni
xii) Kutotii kengele



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xiii) Kuongea kwa lugha isiyo rasmi
xiv) Kutumia njia mbadala shuleni
xv) Kutoheshimu walimu

***Tanbihi***

1. ***Mtahiniwa awe na hoja nane ili kujitosheleza kimaudhui***
2. ***Akikosa sura ya hotuba adhibiwe kwa kutolewa alama nne za sura***

## 2. UFAHAMU

a) Mazingira ni vitu vyote vilivyo na nsivyo na uhai vinavyomzunguka binadamu. **1x2**

b) juhudi za serikali

i) kuanzisha wizara ya mazingira

ii) kutumia mamilioni ya pesa kusafisha mto Nairobi

iii) kuanzisha shirika la mazingira la NEMA **( za kwanza 2 x 1)**

c) mchango wa Prof. Wangari Maathai

i) Alipinga mpango wa serikali wa kujenga jumba katika bustani ya Uhuru.

ii) Aliweka juhudi kulinda msitu wa Karura uliotaka kunyakuliwa na wanabiashara wa makaa na mbao. **2 x 2**

d) i) kutupa taka ovyo

ii) kukata miti kiholela

iii) uteketezaji wa ardhi kwa minajili ya kulima

iv) kemikali kutoka viwandani

v) matumizi ya silaha za kunyukilia ***( za kwanza 4x 1)***

e) fujo/ghasia/fihi/ugomvi **1x1**

f) i) zilifaulu

ii) jukumu/kazi **2x 1**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **ALAMA 40**

a) (i) irabu ya mbele wastani /e/

ii) irabu ya kati chini /a/


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**2 X 1**

b) Kutenga silabi

Tu-nywe-sha-vyo

**3X 1**

c) Ngeli

(i) Kijakazi A-WA

(ii) Malezi U- YA **2 X1**

d) Vipashio ya Lugha

Sauti
Silabi
Neno
Sentensi **4 x 1**

e) Mwanafunzi mwerevu ametuzwa zawadi

Nomino (N) kivumishi (V) kitenzi (T) Nomino (N)

**4x1**

f) Kuweka shadda

i) Da<u>ra</u>sa

ii) <u>Ndo</u>a **2 x 1**

g) i) Sauti mwambatano- sauti zilizo na konsonanti mbili au zaidi na kutamkwa kama sauti moja /nd/ /ngw/

**1x2**

iii) janga /ng/

mbao- /mb/ **2 x1**

h) Majukumu ya lugha

i) Kuelimisha

ii) Kuwasiliana

iii) Kutatua mizozo

iv) Kitambulisho cha jamii

**v)** Huhifadhi utamaduni **3x 1**

i) Miundo ya silabi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mwanao | mwa - | na- | o | |
| | KKI | KI | I | **3 x 1** |

j) Kukanusha



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

i) Tabibu hajamtibu mgonjwa
ii) Kiatu chake hakitanunuliwa kesho **2 x1**

k) i) Kiimbo ni upandaji na ushukaji wa mawimbi ya sauti mtu anapoongea **1x1**

ii) a) Kitabu kimepotea? – swali

b) Kitabu kimepatikana. - Sentensi arifu/taarifa **2 x1**

l) i) kiyeyusho - /w/ /y/

ii) kimadende - /r/ **2 x 1**

m) wingi

i) pahala hapa ni pao
ii) watoto wamenunuliwa vitabu vipya **2x1**

n) Kusahihisha kwa njia tatu

Mahali humu mlimo mna siafu wengi
Mahali huku mliko kuna sifu wengi
Mahali hapa mlipo pana siafu wengi **3 x 1**

o) Mungu ni kwa Maulana na **njia/baraste** ni kwa barabara ilhali banati ni kwa **msichana** **2 x1**

**4. ISIMUJAMII** **ALAMA 10**

a) (i)Sajili ya sokoni/biashara/dukani 2x1

b) sifa za sajili ya sokoni

i) kuchanganya ndimi-freshmatumizi ya msimu-mbao, hamsa

ii) lugha ya ucheshi
iii) kauli fupi

iv) utohozi wa maneno- sketi **4 x 1 (kutaja sifa ½ , mfano ½ )** ***kadiria hoja zaidi za mwanafunzi***

b) kaida za lugha

i) mazingira/ muktadha
ii) uhusiano
iii) jinsia/uana
iv) lengo/madhumuni
v) mada
vi) hali ya mtu
vii) utabaka **za kwanza 4x1**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SEHEMU YA 5 FASIHI SIMULIZI** **ALAMA 15**

1. i) Maana ya fasihi

Ni Sanaa inayotumia lugha kuwakilisha mawazo yanayomhusu binadamu

(1x 2 = 2)

ii. aina za fasihi

a. Fasihi andishi
b. Fasihi simulizi (2 x 1 =2)

Kutofautisha

| **Simulizi** | **Andishi** |
|---|---|
| Njia ya mdomo | Njia ya maandishi |
| Mali ya jamii | Mali ya mwandishi |
| Hadhira hai | Hadhira tuli |

(3x 1 = 3)

2. i) hadhira- wasikilizaji au watazamaji wa kazi ya fasihi

ii) Fanani- mtunzi na mwasilishaji wa kazi ya fasihi simulizi (2 x 1 = 2)

3. vipera vya hadithi

hurafa
hekaya
mighani
ngano za mazimwi
ngano za usuli
visasili (4x1 = 4)

3. Aina za hadhira

Hadhira hai- hadhira inayoshirikishwa
Hadhira tuli-hadhira isiyoshirikishwa
(2 x 1 = 2)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes